

MAKTABA KUU- ZANZIBAR.

KANUNI ZA KUJIUNGA NA UANACHAMA WA MAKTABA.

1. Kila anaetaka kujiunga na uanachama wa maktaba atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo inapatikana katika dawati la mapokezi.
2. Fomu hiyo utatakiwa uirejeshe pamoja ikiwa na picha moja ya stamp (passport size). Itakayotumika katika kutengenezea kitambulisho (IDENTITY CARD) ambacho utatakiwa kuwa nacho unapokuja kupata huduma za maktaba.
3. Fomu hiyo lazima iwe na muhuri halali wa skuli au muhuri wa sheha katika eneo unalotoka.
4. Utatakiwa kuandika namba yako au ya mdhamini wako ya simu ya halali kabisa, itakayotuwezesha kukupata pindi kukiwa na haja ya kufanya mawasiliano na wewe.

GHARAMA ZA UANACHAMA

5. Wanafunzi wa Vyuo TSH 5000/=
6. Wanafunzi wa Secondary FIII – FVI = 3000/=
7. STD VII – FII TSH 2000/=
8. STD I – STD VI TSH 1000/=
9. WENGINEO TSH 5000/=

KWA WAGENI

10. Wanafunzi wa Primary TSH 10,000/=
11. Wanafunzi wa Secondary TSH 15,000/=
12. WENGINEO TSH 20,000/=
13. Uanachama utakaopewa utadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu na utalazimika kuongeza muda wa uanachama uliopewa kwa kulipia nusu gharama ulizolipa wakati wa kuomba uanachama.
14. Kila mwanachama atapatiwa kadi mbili (READERS TICKET) zitakazomuwezesha kuazima vitabu viwili kwa wakati mmoja.

KANUNI ZA UTUMIAJI WA MAKTABA

- 1.Hifadhi mikoba yako katika dawati la mapokezi . ni marufuku kabisa kuingia ndani ya maktaba na mikoba , mifuko au vifurushi.
- 2.Ni wanachama tu ndio watakaoruhusiwa kuazima vitabu na idadi ya mwisho ya vitabu vya kuazima itakua ni viwili (2) kwa wakati mmoja.
- 3.Muda wa kuazima vitabu ni wiki mbili na baadhi ya vitabu ni wiki moja na lazima virudishwe si zaidi ya tarehe iliyoonyeshwa nyuma ya kitabu
- 4.Iwapo mwanachama atahitaji kuongeza muda wa kukaa na kitabu/vitabu ni lazima avirejeshe maktaba kwa kuongezwa muda.
- 5.Atakaecheleweshwa kurejesha kitabu/vitabu atalazimika kulipa faini ya Tsh. 200/-kwa siku kwa kila kitabu na hataruhusiwa kuchukua kitabu kingine akishindwa kulipa faini hiyo na uanachama wake utasimamishwa hadi hapo atakapolipa faini hiyo.
- 6.Ikiwa mwanachama hatotumia uanachama wake kwa mwaka mzima ,uanachama wake huo utakua umefutika.
7. Ni marufuku kuazima kitabu kwa kutumia kadi ya mtu mwingine .
8. Yeyote atakaebainika kuchukua kitabu kwa nia ya kuiba atachukuliwa hatua za kisheria
- 9.Mwanachama atakaepoteza , atakaerudisha kitabu hali ya kuwa kimechanika au kupungua karatasi ,atalazimika kukilipa kitabu hicho.
10. si ruhusa kuzungumza na simu unapokua Maktaba.
- 11.hairuhusiwi kula, kunywa, wala kuvuta sigara ndani ya Maktaba
- 12.Ni mrufuku kufanya majadiliano kwa sauti Kubwa ndani ya Maktaba.

ZINGATIA:

- Unalazimika kufuata kanuni hizi wakati wote unapokuwa maktaba
- Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakevunja sheria hizi

Tunaomba ushirikiano wako

Kurejeshwa kwa fomu hii inathibitisha kuwa umezisoma na kuzifahamu kanuni za utumiaji wa maktaba yetu na upo tayari kuzifuata